# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
## MTIHANI WA TAIFA WA DARASA LA NNE - 2014

**SOMO: KISWAHILI**

**054**

**JINA LA MTAHINIWA: ……………………………………………………………**
**JINA LA SHULE: ………………………………………………………………**
**HALMASHAURI: …………………………………………………………....**
**MKOA: ……………………………………………………………………….**

**MUDA: SAA 1**

**MAELEKEZO:**
1. **Mtihani huu una sehemu tano A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali 25.**
2. **Jibu maswali yote kama ilvyoelekezwa katika kila sehemu.**
3. **Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi zilizotolewa katika kila swali.**
4. **Andika Jina lako, Jina la Shule yako, Halmashauri na Mkoa.**
5. **Simu za mkononi haziruhusiwi kwenye chumba cha Mitihani.**

maktaba.tetea.org
TETEA

Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org/

## SEHEMU: A

**Sikiliza sentensi zinazosomwa kisha uziandike.**

1. ……………………………………………………………………………………………
2. ……………………………………………………………………………………………
3. ……………………………………………………………………………………………
4. ……………………………………………………………………………………………
5. ……………………………………………………………………………………………

## SEHEMU: B

**Jibu swali la 6 – 10 kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika katika kisanduku pembeni ya kila swali.**

6. …………………… likilia kuna jambo.
   A. La polisi
   B. La mtu
   C. La mgambo
   D. La jeshi

7. Mtu anayeendesha ndege huitwa ……………………
   A. rubani.
   B. nahodha.
   C. utingo.
   D. dereva.

8. Ni marufuku mifugo yetu …………………… karibu na Hifadhi za Taifa.
   A. kutembelea
   B. kucheza
   C. kukimbia
   D. kuzurura

9. Watu wengi walilima …………………… ya mto Rufiji.
   A. katikati
   B. kando
   C. ndani
   D. nyuma

10. Ziwa Tanganyika liko upande wa …………………… mwa nchi ya Tanzania.
    A. magharibi
    B. kaskazini
    C. kusini
    D. mashariki



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org/

## SEHEMU: C

**Jibu swali la 11 – 15 kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

11. ……………………. wawili hawakai zizi moja.
12. Asha alimuonea haya mwalimu wake. Onea haya maana yake ni …………………….
13. Ngoja ngoja yaumiza …………………….
14. Watu wengi walivunjika moyo. Kuvunjika moyo maana yake ni …………………….
15. Mchagua jembe si …………………….

## SEHEMU: D

**Katika swali la 16 – 20 umepewa methali na vitendawili. Chagua jibu sahihi kutoka sehemu B na andika herufi ya jibu hilo mbele ya swali katika sehemu A.**

| SEHEMU: A | SEHEMU: B |
|---|---|
| 16. Kuuliza si …………………. | A. wema |
| 17. Popo mbili zavuka mto. …………………. | B. nanasi |
| 18. …………………. la mkuu huvunjika guu | C. limau |
| 19. Kuku wangu katagia mibani …………………. | D. ujinga |
| 20. Kuku mgeni hakosi …………………. mguuni | E. masikio |
| | F. Asiyesikia |
| | G. macho |
| | H. Asiyekubali |
| | I. kamba |
| | J. alama |


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org/

**SEHEMU: E**

**Soma habari ifuatayo kisha jibu swali la 21 – 25.**

Madini ni maliasili inayotupatia fedha nyingi. Tunayo machimbo ya dhahabu na almasi. Pia kuna ulanga na bati. Dhahabu hutumika kutengeneza mapambo kama vile bangili, hereni, mikufu na pete.

Ni vizuri kila mtu aelewe faida ya kutunza kila maliasili tuliyo nayo. Wanyama wakitunzwa huzaliana vizuri. Miti ikitunzwa vizuri hukua haraka. Tukitunza misitu nayo itatutunza. Itatupatia mvua ya kutosha, hewa safi na miti ya mbao na ya kujengea. Tunatakiwa tusubiri muda mrefu vitu vizaliane. Mvumilivu hula mbivu. Tukazane kupanda miti karibu na nyumba zetu ili kuzuia upepo usiharibu mapaa ya nyumba.

**MASWALI:**

21. Kichwa cha habari uliyoisoma ni ……………………………………..……………………….

22. Kutokana na habari uliyoisoma ni madini mangapi yametajwa?
……………………………………………………………………………………………….

23. Bangili, hereni, mikufu na pete hutengenezwa kwa madini gani?
……………………………………………………………………………………………….

23. Taja faida moja tunayopata kutokana na misitu.
……………………………………………………………………………………………….

25. Madini ni maliasili inayotupatia …………………………………………………………….



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org/